**HALMASHAURI YA WILAYA YA MASWA**

**MUHTASARI WA KIKAO CHA TIMU YA MENEJIMENTI YA HALMASHAURI (CMT) CHA ROBO YA KWANZA, 2021/2022 KILICHOFANYIKA TAREHE 13/10/2021 KATIKA UKUMBI MDOGO WA HALMASHAURI YA WILAYA**

**A: WAJUMBE WALIOHUDHURIA**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Bw. Vivian M.Christian | Kaimu Mkurugenzi Mtendaji | Mwenyekiti |
| 2. | Bw. Ahobokile M. Songela | Afisa Rasilimali Watu | Katibu |
| 3. | Bw. Francis K. Johanes | Kaimu Mweka Hazina | Mjumbe |
| 4. | Bw. Vivian M. Christian | Afisa Ardhi na Maliasili | Mjumbe |
| 5. | Bw. Richard Massawe | Mdhibiti na Mkaguzi Ubora wa Shule | Mjumbe |
| 6. | Dkt. James M.Kawamala | Kaimu Afisa Mifugo na Uvuvi | Mjumbe |
| 7. | Bw. Dutu L. Kafula | Kaimu Afisa Mazingira na Taka Ngumu | Mjumbe |
| 8. | Bw. Fidelis Apolinary | Afisa Elimu Sekondari | Mjumbe |
| 9. | Bw. Simon Nyadwera | Kaimu Mtendaji wa M/M/M | Mjumbe |
| 10. | Bi. Mercy D. Ndutu | Kaimu Afisa Maendeleo ya Jamii | Mjumbe |
| 11. | Bw. Charles F. Gatawa | Mkuu wa Chuo cha Binza VTC | Mjumbe |
| 12. | Bw. Isaack G. Matilya | Kaimu Afisa Ugavi | Mjumbe |
| 13. | Bw. Malembo Phinias | Afisa TEHAMA | Mjumbe |
| 14. | Bi. Lucy Kulong'wa | Afisa Elimu Msingi | Mjumbe |
| 15. | Bi. Anna E. Tirutoza | Afisa Uchaguzi | Mjumbe |
| 16. | Bi. Scola Kisibo | Mwanasheria | Mjumbe |
| 17. | Bw. Robert E. Urassa | Afisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika | Mjumbe |
| 18. | Eng. Msoka Msumba | Mhandisi wa Ujenzi | Mjumbe |
| 19. | Bw. Anthony P. Maganga | Kaimu Afisa Nyuki | Mjumbe |



Scanned with CamScanner

| | | | |
|---|---|---|---|
| 20. | Bw. Ghalib Mkumbwa | Kaimu Afisa Mipango | Mjumbe |
| 21. | Bw. Rimoy C. Marley | Kaimu Mkaguzi wa Ndani | Mjumbe |
| 22. | Bw. Abel M. Machibya | Kaimu Mganga Mkuu | Mjumbe |
| 23. | Bw. Amon M. Nhindilo | Katibu TSC | Mjumbe |
| 24. | Bw. Damas Maregesi | Kaimu Mratibu TASAF | Mjumbe |
| 25. | Bw. Saguda E. Sayayi | Kaimu Katibu Tawala | Mjumbe |

**B: WAJUMBE WASIOHUDHURIA KWA TAARIFA**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Bw. James Rweyemamu | Afisa Utamaduni | Mjumbe |

**C: SEKRETARIETI**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Bw. Peter K. Charles | Mwandishi wa Kikao |

**D: AGENDA ZA KIKAO**

1. Kufungua kikao;
2. Kuthibitisha agenda za Kikao;
3. Kusoma na kuthibitisha Muhtasari wa kikao kilichopita cha tarehe 15/09/2021;
4. Yatokanayo na kikao cha tarehe 15/10/2021;
5. Kusoma Muhtasari wa kikao cha Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango kilichopita ch tarehe 20/09/2021 na yatokanayo na kikao hicho;
6. Taarifa ya Mapato na Matumizi kwa kipindi cha kuishia mwezi Septemba, 2021;
7. Taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika kipindi cha Julai hadi Septemb 2021/2022;
8. Taarifa ya utekelezaji ya idara ya Utawala na Utumishi kwa kipindi cha Julai h Septemba, 2021/2022;
9. Taarifa ya mpango wa kunusuru kaya maskini TASAF III kwa kipindi cha Julai h Septemba, 2021/2022;



Scanned with CamScanner

10. Taarifa ya Manunuzi kwa kipindi cha Julai hadi Septemba, 2021/2022;
11. Taarifa ya utekelezaji wa Chuo cha Binza VTC kwa kipindi cha Julai hadi Septemba, 2021/2022;
12. Taarifa ya utekelezaji wa dawati la Malalamiko na Msaada kwa wateja kwa kipindi cha Julai hadi Septemba, 2021/2022;
13. Taarifa ya utekelezaji wa mradi wa kilimo cha kisasa kwa njia ya kitalu nyumba (Green House)
14. Taarifa ya Mapokezi ya fedha za UVIKO 19 kiasi cha Tsh. 2,130,000,000/=
15. Taarifa ya utekelezaji wa zoezi la chanjo ya SOTOKA ya wanyama wadogo (Peste Des Petits Ruminants)
16. Taarifa ya vipaumbele vya miradi ya maendeleo;
17. Makabidhiano ya tenki la maji Nyalikungu;
18. Kufunga kikao.

**AGENDA CMT NA 14/09/2021: KUFUNGUA KIKAO;**

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti ili aweze kufungua kikao ambapo Mwenyekiti alifungua kikao saa **1:30** asubuhi akiwaomba wajumbe kujadili kwa umakini agenda ambazo ziliwasilishwa katika kikao hicho kwa ajili ya manufaa ya Halmashauri.

**AGENDA CMT NA 15/09/2021: KUTHIBITISHA AGENDA ZA KIKAO;**

Mwenyekiti aliwaomba wajumbe kuthibitisha agenda ambazo ziliwasilishwa mbele yao. Wajumbe walipitia agenda moja baada ya nyingine na hapakuwepo na ongezeko la agenda, wajumbe walithibitisha na kuridhia kuwa agenda sahihi za kikao.



Scanned with CamScanner

**AGENDA CMT NA 16/09/2021: KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO KILICHOPITA CHA TAREHE 15/09/2021;**

Mwenyekiti aliwaomba wajumbe waupitie Muhtasari wa kikao kilichopita cha tarehe 15/09/2021 ukurasa kwa ukurasa na pakawepo na masahihisho kama ifuatavyo:-

1) Ukurasa wa 3 halisi isomeke sahihi
2) Ukurasa wa 1 hadi 2 majina ya wajumbe yaandikwe matatu
3) Ukurasa wa 8 faidia isomeke faida
4) Ukurasa wa 8 alishauri isomeke walishauri

Baada ya masahihisho hayo wajumbe waliridhia muhtasari usainiwe na Mwenyekiti na Katibu ili uweze kuwa kumbukumbu sahihi ya Halmashauri.

**AGENDA CMT NA 17/09/2021: YATOKANAYO NA KIKAO CHA TAREHE 15/09/2021**

Taarifa ya utekelezaji wa maazimio ya kikao kilichofanyika tarehe 15/09/2021 iliwasilishwa na katibu kama ifuatavyo:-

1. Katika kikao kijacho, Wakuu wa idara na Vitengo wabainishe madeni yote ya manunuzi yaliyolipwa na yale ambayo hayajalipwa ili kusaidia kuweka vizuri kumbukumbu za madeni hayo ikiwa ni pamoja na kuhakikisha madeni hayo yanalipwa. Agizo halikutekelezwa, wajumbe waliagiza utekelezaji ufanyike na tarehe 13/10/2021 saa 5:00 asubuhi kila mkuu wa idara awasilishe madeni yote ya wazabuni na madeni ya watumishi katika ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji.

**Azimio:-** Ifikapo saa 5:00 asubuhi ya tarehe 13/10/2021 kila mkuu wa idara awasilishe madeni yote ya wazabuni na madeni ya watumishi katika ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji.



Scanned with CamScanner

2. Mwanasheria, Mweka Hazina na Mtendaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo wafuatilie deni la kiasi cha **Tsh. 28,000,000/=** walilokubaliana Maswa Family kulipa deni hilo kama wapangaji wa jengo la Halmashauri kwa mujibu wa Mkataba. Agizo halikutekelezwa, wajumbe waliagiza utekelezji ufanyike na katika kikao kijacho majibu kamili ya utekelezaji yawasilishwe.

**Azimio:-** Mwanasheria, Mweka Hazina na Mtendaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo wafuatilie deni la kiasi cha **Tsh. 28,000,000/=** walilokubaliana Maswa Family kulipa deni hilo kama wapangaji wa jengo la Halmashauri kwa mujibu wa Mkataba.

**AGENDA CMT NA 18/09/2021: KUSOMA MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA UTAWALA NA MIPANGO KILICHOPITA CHA TAREHE 20/09/2021 NA YATOKANAYO NA KIKAO HICHO;**

Muhtasari wa kamati ya fedha Utawala na Mipango wa tarehe 20/09/2021 ulisomwa mbele ya wajumbe na Mwenyekiti aliwaomba wajumbe waupitie Muhtasari huo kwa ajili ya masahihisho na pakawepo na masahihisho kama ifuatavyo:-

1. Ukurasa wa 8 mathubuti isomeke madhubuti.

Aidha wajumbe walipitia maazimio ya kikao hicho kama ifuatavyo:-

1. Mwanzoni mwa mwezi Oktoba, 2021 Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango ifanye ziara ya kwenda katika kiwanda cha viatu kilichopo katika manispaa ya Moshi kwenda kujifunza namna ya uendeshaji wa viwanda badala ya kwenda Mkalama Mkoani Singida ambako tayari Halmashauri ina leseni ya uchimbaji wa madini ya Gypsum. Maandalizi ya safari yanaendelea kufanyika na endapo yakikamilika safari itafanyika.



Scanned with CamScanner

Wajumbe walijadili na kushauri kuwa wakuu wa idara na vitengo wote waende katika ziara hiyo kwa lengo la kwenda kujifunza kwa sababu wao ndo wasimamizi wa shughuli za maendeleo.

2. Mikakati madhubuti ya kuhakikisha eneo la Maegesho ya magari lililopo katika eneo la Biafra B linaendelezwa iwasilishwe katika kikao kijacho. Agizo lilitekelezwa, mikakati, mapendekezo na ushauri uliwasilishwa. Wajumbe walijadili na kupendekeza kuwa eneo la stendi ya Njiapanda liendelezwe ili liweze kuwa eneo la maegesho ya magari.
3. Taarifa ya Magari yote ya Halmashauri yakiwemo malori iwasilishwe katika kikao kijacho ili wajumbe waweze kushauri namna ya kutengeneza magari hayo ili yaweze kutumika kuongeza mapato ya Halmashauri. Agizo lilitekelezwa, taarifa ya magari iliwasilishwa. Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe walijadili na kushauri kuwa ni vyema magari yote yakatengenezwa na kama Halmashauri haiwezi kutengeneza magari ni vyema sasa magari ambayo ni ya muda mrefu yakauzwa. Aidha, wajumbe waliendelea kujadili na kupendekeza kuwa Halmashauri itengeneze angalau magari machache machache ili yaweze kusaidia utekelezaji wa shughuli za Halmashauri. Vile vile wajumbe walishauri kuwepo na fundi mkuu.

**Azimio:-** Halmashauri iweke mikakati ya kutengeneza magari angalau machache ili yaweze kusaidia utekelezaji wa shughuli za Halmashauri kwa kuanza na magari STK 7089, DFP 8471 na DFP 9263.

**AGENDA CMT NA 19/09/2021: TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA KIPINDI CHA KUISHIA MWEZI SEPTEMBA, 2021;**

Kaimu Mweka Hazina aliwasilisha taarifa ya mapato na matumizi kwa kipindi cha kuishia mwezi Septemba, 2021 kama ifuatavyo.



Scanned with CamScanner

**A: Muhtasari wa Mapato;**

Kwa mwaka wa fedha, 2021/2022 Halmashauri ilikisia kukusanya kiasi cha **Tsh. 42,277,672,730.40.** Hadi kufikia mwezi Septemba 30,2021 kiasi cha **Tsh. 8,199,382,745.35** sawa na asilimia **19.39** kilikuwa kimekusanywa kwa mchanganuo ufuatao:-

| NA | MAELEZO | MAKISIO 2021/2022 | JUMLA YA MAPATO JULAI, 2021 –AGOSTI 2021 (TSH.) | MAPATO HALISI MWEZI SEPTEMBA, 2021 (TSH) | JUMLA YA MAPATO JULAI, 2021 HADI SEPTEMBA, 2021 (TSH) | TOFAUTI (TSH) | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | VYANZO VYA NDANI | 2,251,512,231.40 | 702,108,831.76 | 230,238,267.14 | 932,347,098.90 | 1,319,165,132.50 | 41.41 |
| 2 | MATUMIZI MENGINEYO – OC | 1,046,967,000.00 | 305,225,081.97 | 48,820,667.34 | 354,045,749.31 | 692,921,250.69 | 33.82 |
| 3 | MISHAHARA | 24,833,966,000.00 | 3,903,819,000.00 | 1,936,987,000.00 | 5,840,806,000.00 | 18,993,160,000.00 | 23.52 |
| 4 | MIRADI YA MAENDELEO | 14,145,227,499.00 | 763,136,150.02 | 309,047,747.16 | 1,072,183,897.18 | 13,073,043,601.82 | 7.58 |
| | **JUMLA** | **42,277,672,730.40** | **5,674,289,063.75** | **2,525,093,681.64** | **8,199,382,745.39** | **34,078,289,985.01** | **19.39** |

**B. MUHTASARI WA MATUMIZI;**

Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Halmashauri ilikisia kutumia kiasi cha **Tsh. 42,277,672,730.40**. Hadi kufikia Septemba, 30, 2021 kiasi cha **Tsh. 7,522,140,778.81** sawa na asilimia **17.79** kilikuwa kimetumika kwa mchanganuo ufuatao:-



Scanned with CamScanner

| MAELEZO | MAKISIO 2021/2022 | JUMLA YA MATUMIZI JULAI, 2021 HADI AGOSTI, 2021 | MATUMIZI HALISI MWEZI SEPTEMBA, 2021 | JUMLA YA MATUMIZI JULAI 2021 HADI SEPTEMBA, 2021 | TOFAUTI | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| VYANZO VYA NDANI | 1,628,468,090.04 | 346,306,260.78 | 187,094,853.00 | 533,401,113.78 | 1,095,066,976.26 | 32.75 |
| MATUMIZI ` MENGINEYO –OC | 1,046,964,503.00 | 38,050,404.00 | 38,458,000.00 | 76,508,404.00 | 970,456,099.00 | 7.31 |
| MISHAHARA | 24,833,968,497.00 | 3,903,819,000.00 | 1,936,987,000.00 | 5,840,806,000.00 | 18,993,162,497.00 | 23.52 |
| MIRADI YA MAENDELEO/ MAPATO YA NDANI | 623,044,141.36 | 88,260,000.00 | 34,750,000.00 | 123,010,000.00 | 500,034,141.36 | 19.74 |
| MIRADI YA MAENDELEO/ WAHISANI | 14,145,227,499.00 | 789,776,575.01 | 158,638,686.02 | 948,415,261.03 | 13,196,812,237.97 | 6.70 |
| **JUMLA** | **42,277,672,730.40** | **5,166,212,239.79** | **2,355,928,539.02** | **7,522,140,778.81** | **34,755,531,951.59** | **17.79** |

## C: MAELEZO YA MAPATO YATOKANAYO NA VYANZO VYA NDANI VYA HALMASHAURI;

### i. Malinganisho ya mapato ya ndani ya mwaka 2021/2022

mashauri ilikisia kukusanya jumla ya **Tsh. 2,251,512,231.40** katika mwaka wa fedha 2021/2022 okana na vyanzo vya mapato ya ndani. Kwa kipindi cha Septemba 2021 jumla ya n. **932,347,098.90** zimekusanywa sawa na asilimia **41.41** ya lengo kwa mchanganuo ufuatao:-

| MWAKA | MAKISIO | JUMLA YA MAPATO JULAI, 2020 –JULAI - AGOSTI, 2021 | MAPATO SEPTEMBA, 2021 | JUMLA YA MAPATO JULAI, 2021 – SEPTEMB, 2021 | TOFAUTI | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2021/2022 | 2,251,512,231.40 | 702,108,831.76 | 230,238,267.14 | 932,347,098.90 | 1,319,165,132.50 | 41.41 |
| 2020/2021 | 3,395,561,001.55 | 487,692,125.00 | 247,835,947.00 | 735,528,072.00 | 2,660,032,929.55 | 21.66 |
| **TOFAUTI** | **(1,144,048,770.15)** | **214,416,706.76** | **(17,597,679.86)** | **196,819,026.90** | **(1,340,867,797.05)** | **19.75** |



Scanned with CamScanner

Mapato haya yakilinganishwa na makusanyo ya mwezi Septemba, 2020 yameshuka kwa **Tsh. 17,597,679.86.** Aidha, makusanyo hadi kufikia mwezi Septemba, 2021 yako juu kwa jumla ya **Tsh. 196,819,026.90.**

### ii. MAELEZO YA MAPATO NA MATUMIZI - FEDHA ZA MAPATO YA NDANI KWENYE MIRADI YA MAENDELEO

Halmashauri ilikisia kutumia fedha za mapato ya ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo kiasi cha **Tsh. 623,044,141.36** katika mwaka wa fedha 2021/2022. Hadi kufikia mwezi Septemba, 2021 jumla ya **Tsh. 123,010,000.00** sawa na asilimia **19.74** ya makisio kilikuwa kimetumika kwa ajili ya shughuli za miradi ya maendeleo kama ifuatavyo:-



Scanned with CamScanner

| NA | MAELEZO | MAKISIO | JUMLA YA MATUMIZI JULAI, 2021 – AGOSTI, 2021 | MATUMIZI HALISI MWEZI SEPTEMBA, 2021 | JUMLA YA MATUMIZI JULAI, 2021- SEPTEMBA, 2022 | TOFAUTI | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | MIRADI YA MAENDELEO | 623,044,141.36 | 88,260,000.00 | 34,750,000.00 | 123,010,000.00 | 500,034,141.36 | 19.74 |
| **JUMLA** | | **623,044,141.36** | **88,260,000.00** | **34,750,000.00** | **123,010,000.00** | **500,034,141.36** | **19.74** |

## D. MAELEZO YA BAKAA YA MWAKA WA FEDHA 2020/2021;

Kwa mwaka wa fedha, 2020/2021 Halmashauri ilibakiwa na kiasi cha **Tsh. 2,020,072,198** ikiwa ni fedha za Bakaa ya Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia mwezi Septemba, 2021 kiasi cha **Tsh. 1,339,290,592.77** sawa na asilimia 66.3**0** kilikuwa kimetumika kwa mchanganuo ufuatao:-

| NA | MAELEZO | MAKISIO | JUMLA YA MATUMIZI JULAI, 2021 HADI SEPTEMBA, 2021 | MATUMIZI HALISI MWEZI SEPTEMBA, 2021 | JUMLA YA MATUMIZI JULAI, 2021 HADI SEPTEMBA, 2021 | TOFAUTI | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | BAKAA | 2,020,072,198.00 | 276,813,191.09 | 1,062,477,401.68 | 1,339,290,592.77 | 680,781,605.23 | 66.30 |
| **JUMLA** | | **2,020,072,198.00** | **276,813,191.09** | **1,062,477,401.68** | **1,339,290,592.77** | **680,781,605.23** | **66.30** |

## E: SALIO LA FEDHA HADI TAREHE 30 SEPTEMBA, 2021

Taarifa ilionesha kiasi cha fedha kilichokuwa katika akaunti mbalimbali za Halmashauri ya wilaya kwa kipindi cha kuishia tarehe 30, Septemba, 2021 kuwa ni **Tsh. 1,655,844,826.21.** Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe waliipokea na kubaina kuwa kuna marekebisho ya taarifa ambapo wajumbe walishauri Mweka Hazina, Mkaguzi wa Ndani na Afisa Mipango wakaei ili waweze kufanya marekebisho ya taarifa kabla ya kuwasilishwa katika kikaocha Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango.



Scanned with CamScanner

**AGENDA CMT NA 20/09/2021: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA JULAI HADI SEPTEMBA MWAKA 2021/2022;**

Kaimu Afisa Mipango aliwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa miradi ya Maendeleo kwa kipindi cha robo ya kwanza mwaka 2021/2022 kwa kueleza kuwa katika mwaka wa fedha 2021/2022 Halmashauri ya wilaya iliidhinishiwa kutumia jumla ya **Tsh. 14,768,271,640** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo, Aidha aliongeza kuwa kwa kipindi cha robo ya kwanza (Julai, 2021 hadi Septemba,2022) Halmashauri imepokea kiasi cha **Tsh 806,509,275** sawa na asilimia **5.46** ya fedha iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kwa ajili ya shughuli za miradi ya maendeleo. Aliongeza kuwa hadi kufikia mwishoni mwa robo ya kwanza (Julai, 2021 hadi Septemba, 2022) Halmashauri imepokea kiasi cha **Tsh. 1,181,723,201** nje ya bajeti (yaani **Tsh. 350,000,000** serikali kuu, **Tsh. 739,000,000 EP4** na **Tsh. 92,723,200.54** fedha za COVID 19 kwa ajili ya uhamasishaji wa chanjo na ujenzi wa miundombinu ya maji shule za msingi. Kwa kipindi cha robo ya kwanza 2021/2022 kiasi cha Tsh. 702.378,421 kimetumia kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo Wilayani sawa na asilimia **4.75** ya fedha iliyoidhinishwa.

Aidha, kwa mwaka wa fedha, 2020/2021 Halmashauri ilivuka na jumla ya **Tsh. 2,020,072,198** na hadi Septemba, 2021 jumla ya **Tsh. 1,339,290,592.77** zilikuwa zimetumika sawa na asilimia **14.23**. Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe waliipokea na kushauri marekebisho yafanyike kwa kulinganisha na taarifa ya mapato na matumizi kabla ya taarifa kuwasilishwa katika kikao cha Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango.



Scanned with CamScanner

**AGENDA CMT NA 21/09/2021: TAARIFA YA IDARA YA UTAWALA NA UTUMISHI KWA KIPINDI CHA JULAI HADI SEPTEMBA MWAKA WA FEDHA 2021/2022;**

Kaimu Afisa Utumishi aliwasilisha taarifa ya Idara ya Utumishi na Utawala kwa kipindi cha robo ya kwanza mwaka 2021/2022, taarifa ilionesha jumla ya watumishi waliohama ni **21**, kwa kipindi cha Julai hadi Septemba, 2021/2022 watumishi **5** ndio wamehamia katika Taasisi zingine, watumishi waliostaafu ni **10**, watumishi walioajiriwa kwa kipindi cha Julai hadi Septemba, 2021/2022 ni watumishi **74,** watumishi walioko masomoni ni **55,** kwa kipindi cha Julai hadi Septemba, 2021/2022 watumishi **2** wamefariki dunia, kwa kipindi cha Julai hadi Septemba, 2021/2022 hakuna mtumishi yeyote aliyefunguliwa kesi mahakamani kwa makosa mbalimbali, kwa kipindi cha Julai hadi Septemba, 2021/2022 hakuna mtumishi aliyeacha kazi, kwa kipindi cha Julai hadi Septemba, 2021/2022 hakuna watumishi waliofukuzwa kazi, kwa kipindi cha Julai hadi Septemba, 2021/2022 hakuna mtumishi aliyesimamishwa kazi kwa makosa mbalimbali, kwa kipindi cha Julai hadi Septemba, 2021/2022 hakuna watumishi wapya walioajiriwa. Aidha, aliwasilisha majukumu mbalimbali yaliyotekelezwa na idara ya Utawala, changamoto na mikakati ya kutatua changamoto. Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe waliipokea na kuendelea na agenda iliyofuata.

**AGENDA CMT NA 22/09/2021: TAARIFA YA MPANGO WA KUNUSURU KAYA MASKINI UNAOTEKELEZWA NA TASAF III KWA KIPINDI CHA JULAI HADI SEPTEMBA, 2021/2022;**

Kaimu Mratibu wa TASAF aliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa mpango wa kunusuru kaya maskini kupitia TASAF III kwa kipindi cha Julai hadi Septemba, 2021/2022 wilayani Maswa. Katika kipindi cha Julai hadi Septemba, 2021/2022, uhawilishaji fedha haujafanyika kwa sababu hakuna fedha iliyopokelewa kwa ajili ya kuendesha zoezi la uhawilishaji fedha kwa walengwa na badala yake kiasi cha **Tsh. 915,000/=** zimepokelewa kwa ajili ya zoezi la ukaguzi wa nje kwa mwaka 2020/2021.



Scanned with CamScanner

Taarifa ilielezea shughuli zilizofanyika, changamoto na namna ya kutatua changamoto hizo. Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe waliipokea na kuendelea na agenda iliyofuata.

**AGENDA CMT NA 23/09/2021: TAARIFA YA MANUNUZI KWA KIPINDI CHA JULAI HADI SEPTEMBA MWAKA WA FEDHA 2021/2022;**

Kaimu Afisa Ugavi aliwasilisha Taarifa ya Manunuzi kwa kipindi cha robo ya kwanza - Julai hadi Septemba, 2021/2022 ambapo taarifa ilikuwa imegawanyika katika sehemu kuu nne mbili (2) ambazo ni Manunuzi kupitia bodi ya zabuni na Manunuzi kwa njia ya mikataba midogo (P.O). Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe waliipokea taarifa na kuendelea na agenda iliyofuata.

**AGENDA CMT NA 24/09/2021: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA CHUO CHA BINZA VTC KWA KIPINDI CHA JULAI HADI SEPTEMBA, 2021/2022;**

Mkuu wa chuo cha Binza VTC aliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa chuo cha Binza VTC kwa kipindi cha Julai hadi Septemba, 2021/2022. Taarifa ilieleza kuwa Chuo cha Binza VTC kimeweza kukusanya Jumla ya **Tsh. 68,720,940.00** katika mwaka wa fedha, 2021/2022 kutokana na vyanzo mbalimbali vya mapato. Aliendelea kueleza kuwa hadi kufikia Mwezi Septemba, 2021 chuo kimekwisha tumia kiasi cha **Tsh. 81,292,186.96** katika kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo. Aidha, taarifa ilieleza shughuli mbalimbali zilizotekelezwa na chuo hicho kwa kipindi cha Julai hadi Septemba, 2021/2022, Changamoto na Mikakati ya kutatua changamoto hizo. Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe waliipokea na kuendelea na agenda iliyofuata.

**AGENDA CMT NA 25/09/2021: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA DAWATI LA MALALAMIKO NA MSAADA KWA WATEJA KWA KIPINDI CHA JULAI HADI SEPTEMBA, 2021/2022**

Afisa Uchaguzi aliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa shughuli za dawati la malalamiko na msaada kwa wateja kwa kipindi ca Julai hadi Septemba, 2021/2022.



Scanned with CamScanner

Taarifa ilieleza kuwa katika kipindi cha robo ya kwanza jumla ya kero 4 zimewasilishwa katika dawati la malalamiko na kutafutiwa ufumbuzi.

Aidha, kero/malalamiko hayo yalihusisha idara ya Ardhi na Maliasili, idara ya Elimu Msingi, idara ya utumishi na Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Mjini. Aidha, taarifa ilieleza changamoto na mikakati ya kutatua changamoto hizo. Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe walishauri Ofisi ya Malalamiko inatakiwa ijulikane kuwa inapatikana sehemu gani kwa hapa Halmashauri ili wananchi waweze kuifahamu na kuwasilisha malalamiko/kero zao.

**AGENDA CMT NA 26/09/2021: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MRADI WA KILIMO CHA KISASA KWA NJIA YA KITALU NYUMBA (GREEN HOUSE)**

Afisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika aliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa mradi wa kilimo cha kisasa kwa njia ya Kitalu Nyumba yaani Green House kwa kueleza kuwa wilaya ilipokea barua yenye kumb. Na. CA.9/263/210/01"Q"/42 ya mwezi Septemba, 2018 toka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ikielekeza kutenga eneo kwa ajili ya kilimo cha Umwagiliaji kwa kutumia teknolojia ya kitalu nyumba (Green House).

Hata hivyo wilaya kwa kushirikiana na Kampuni ya Royal AGRIC Co. LTD ilianza kutekeleza mradi huu mnamo tarehe 04/02/2019 kwa kufundisha vijana kujenga kitalu nyumba ambapo katika awamu ya kwanza ilikamilika na mnamo tarehe 08/02/2019 vijana wapatao 19 kati yao wasichana 5 na wavulana 14 walipata mafunzo hayo.

Aidha, taarifa ilieleza kuwa wilaya kwa kushirikiana na kampuni hiyo ya Royal AGRIC Co. LTD iliendelea na mafunzo kwa vijana 80 ambapo vijana 11 ni wenye ulemavu wa viungo. Mafunzo hayo yalikuwa juu ya kilimo cha kutumia teknolojia ya kitalu nyumba.

Vile vile taarifa ilieleza gharama ya ujenzi wa kitalu nyumba zilizochangiwa na Halmashauri, Hali ya mradi kwa sasa, changamoto na mikakati ya kutatua changamoto hizo.



Scanned with CamScanner

Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe walishauri eneo hilo lizungushiwe uzio, aidha, tusimamie marejesho ya mkopo huo pamoja na kusimamia mradi huo kwa ukaribu kwa kuangalia watu wenye nia na mradi.

**AGENDA CMT NA 27/09/2021: TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA ZA UVIKO 19 KIASI CHA TSH. 2,130,000,000/=**

Kaimu Afisa Mipango aliwasilisha taarifa ya mapokezi ya fedha za Uviko 19 kiasi cha **Tsh. 2,130,000,000/=** zilizopokelewa kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya Maendeleo. Aidha, aliendelea kueleza kuwa kati ya fedha hizo zilizopokelewa kiasi cha **Tsh. 1,400,000,000/=** kwa ajili ya ujenzi wa vyumba **(70)** vya madarasa kwa shule za sekondari, kiasi cha **Tsh. 260,000,000/=** ni fedha kwa ajili ya ujenzi wa shule shikizi tano (5) kwa madarasa (13), kiasi cha **Tsh. 80,000,000/=** kwa ajili ya ujenzi wa bweni la mahitaji maalum, kiasi cha **Tsh. 90,000,000/=** kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya mtumishi (3 in 1) na kiasi cha **Tsh. 300,000,000/=** kwa ajili ya ujenzi wa jengo la dharura (EMD). Baada ya taarifa ya mapokezi ya fedha hizo kuwasilishwa wajumbe waliipokea na kushauri mchakato wa hatua za utekelezaji wa miradi hiyo uendelee.

**AGENDA CMT NA 28/09/2021: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA ZOEZI LA CHANJO YA SOTOKA YA WANYAMA WADOGO (PESTE DES PETITS RUMINANTS)**

Kaimu Afisa Mifugo na Uvuvi aliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa zoezi la chanjo ya SOTOKA ya wanyama wadogo kwa kueleza kuwa, Halmashauri ya wilaya ya Maswa ilipokea dozi **50,000** za chanjo ya ugonjwa wa Sotoka ya wanyama wadogo kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi wa ajili ya kuchanja mbuzi na kondoo dhidi ya ugonjwa wa PPR.



Scanned with CamScanner

Zoezi la utoaji wa chanjo hizo limefanyika katika jumla ya Kata 29 na hadi kufikia tarehe 30/09/2021 jumla ya mbuzi 27,688 na Kondoo 15,224 walikuwa wamechanjwa kati ya mbuzi 106,974 na kondoo 61,128 wanaokadiriwa kuwepo sawa na asilimia 25.53 ya Mbuzi na Kondoo wote waliopo.

Aidha, Jumla ya Tsh. 15,019,200/= zilikusanywa. Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa wajumbe waliipokea na kuridhia zoezi liendelee.

Taarifa ilieleza changamoto na mikakati ya kutatua changamoto hizo. Baada ya taarifa kuwasilishwa, wajumbe waliipokea na kuendelea na agenda iliyofuata.

**AGENDA CMT NA 29/09/2021: TAARIFA YA VIPAUMBELE VYA MIRADI YA MAENDELEO;**

Kaimu Afisa Maendeleo ya Jamii aliwasilisha vipaumbele vya miradi ya maendeleo kwa kueleza kuwa wilaya ya Maswa imebahatika kupitiwa na mradi mkubwa wa Kimkakati wa ujenzi wa reli ya mwendo kasi ambapo utapita katika vijiji vya Ikungu, Nyashimba (S), Malampaka, Gulung'washi, Lali na Mwabagalu. Katika utekelezaji wa mradi huo wa kimkakati kampuni husika husaidia utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika vijiji husika (CSR) kwa mujibu wa sharia.

Uongozi wa kampuni ulifika katika Halmashari ya wilaya kwa ajili ya kuhitaji vipaumbele vya miradi ya maendeleo kwenye vijiji ambavyo mradi huo utapita.

Aliwasilisha vipaumbele vya Afya, elimu sekondari, elimu msingi na maendeleo ya Jamii ili wajumbe waweze kujadili/kushauri pamoja na kuridhia vipaumbele hivyo. Baada ya vipaumbele hivyo kuwasilishwa wajumbe walishauri wananchi washirikishwe katika kuibua miradi, vilevile wajumbe walishauri kuwa ni vyema tukafahamu bajeti ya kampuni katika ujenzi wa miundombinu kabla ya kuibua miradi.



Scanned with CamScanner

**AGENDA CMT NA 30/09/2021: MAKABIDHIANO YA TENKI LA MAJI NYALIKUNGU;**

Afisa Ardhi na Maliasili aliwasilisha taarifa ya makabidhiano ya tenki la maji Nyalikungu kutoka Halmashauri ya wilaya ya Maswa kwenda MAUWASA. Taarifa ilieleza kuwa mnamo tarehe 20/08/2021 Kamati ya Siasa ya Mkoa wa Simiyu ilifanya ziara ya kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo iliyotekelezwa na inayoendelea kutekelezwa katika wilaya ya Maswa. Kamati ya Siasa ilikagua miradi katika sekta ya Afya, Viwanda, Maji, Elimu na Barabara.

Katika ziara hiyo Kamati ilitembelea mradi wa maji ambao ujenzi wake unatekelezwa na Mamlaka ya Maji Maswa Mjini (MAUWASA) ambapo pia ilibainika uwepo wa tanki la maji ambalo halitumiki ili hali ujenzi wa tanki linguine ukiendelea.

Kufuatia taarifa hiyo Mkuu wa Mkoa wa Simiyu Mhe. David Kafulila alitoa agizo kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya ya Maswa kuandaa taarifa ya mradi huo na kuiwasilisha Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ndani ya siku saba.

Kutokana na kutokuwepo kwa wahandisi wa maji katika ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji, ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji iliamua kuunda timu ya wataalam watano kwa lengo la kufanya uchunguzi wa kitaalam kujua sababu ya tanki hilo kutokufanya kazi na kutoa maoni yao ya kitaalam ya nini kifanyike ili tanki hilo liweze kutumika.

Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa Mkoani yalitolewa maelekezo kuwa mradi huo wa tanki la maji Nyalikungu ukabidhiwe Mamlaka ya Maji Maswa Mjini (MAUWASA).

Tayari hati ya Makabidhiano imeandaliwa. Taarifa hiyo iliwasilishwa katika kikao cha Menejimenti ili kuweza kuridhia maelekezo hayo. Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe waliipokea na kuridhia tenki hilo likabidhiwe Mamlaka ya Maji Maswa Mjini (MAUWASA).

**AGENDA CMT NA 31/09/2021: KUFUNGA KIKAO.**

Mwenyekiti alifunga kikao saa 6:35 mchana akiwashukuru wajumbe kwa michango yao na mwisho aliwatakia mchana mwema.



Scanned with CamScanner

**UMETHIBITISHWA NA:-**

| | |
|---|---|
| ……………………………… | ……………………………… |
| MWENYEKITI | KATIBU |
| TAREHE ……15/11/2021…… | TAREHE……15/11/2021…… |



Scanned with CamScanner